

**Swali:** Katika kitabu cha *Matendo 13:1*, tunamsoma mtu mmoja akitajwa kama ndugu wa kunyonya wa Herode, je maana yake nini?.

---

**Jibu:** Maana ya “**Ndugu wa kunyonya**” ni “**mtu aliyelelewa katika familia fulani, tangu utotoni, alipokuwa akinyonya**” kwa lugha nyingine amekuwa “adopted” tangu utotoni, (*katika umri wa kunyonya*).

Hivyo mtu kama huyu anahesabika kuwa kama mwanafamilia, na watoto wa familia hiyo watamhesabu kama ndugu yao wa kunyonya, kwani amekulia katika familia yao.

Hivyo huyu Manaeni alilelewa pamoja na Mfalme Herode, katika familia moja, ingawa hawakuwa ndugu wa damu, lakini tangu utoto walikuwa pamoja.

*Matendo 13:1 “Na huko Antiokia katika kanisa lililokuwako palikuwa na manabii na waalimu, nao ni Barnaba, na Simeoni aitwaye Nigeri, na Lukio Mkirene, na MANAENI ALIYEKUWA NDUGU WA KUNYONYA WA MFALME HERODE, na Sauli”.*

Lakini kulikuwa na kusudi kwanini habari zake ziandikwe katika biblia, ukizingatia ya kuwa ndugu yake, ambaye alikuwa ni Herode pamoja na maherode wote walikuwa ni wakatili sana, waliwaua wakristo na kuwapiga vita vikali, lakini huyu Manaeni ambaye ni ndugu ya Herode, yeye alikuwa wa tofauti, kwani alikuwa ni miongoni mwa watu wa kwanza kabisa kugeuka na kuifuata Imani ya Kikristo, na kuwa miongoni mwa wasimamizi wa Imani katika kanisa la kwanza la watu wa mataifa, huko Antiokia.

Na kumbuka Antiokia ndiko jina la Ukristo lilikozaliwa, kwani hapo kabla waliomfuata YESU walikuwa wanaitwa wanafunzi tu.

*Matendo 11: 26 "hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia"*

Sasa kufahamu kwa urefu ushuhuda alilolibeba Mtumishi huyu wa Mungu (Manaeni) na ujumbe tuupatao watu wa sasa katika Kanisa, fungua hapa >>> **NI NINI TUNAJIFUNZA KWA YOANA NA MANAENI?**

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

### **Mafundisho mengine:**

**[Antiokia ni wapi kwasasa?](#)**

**[NI NINI TUNAJIFUNZA KWA YOANA NA MANAENI?](#)**

**[Mimbari ni nini? Je tofauti kati ya Mimbari na madhabahu ni ipi?](#)**

**[Nini maana ya “Atamwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake”.](#)**

Biblia inaposema ndugu wa kunyonya inamaanisha nini (Matendo  
13:1)?

**(2Wathesalonike 2:8).**

**Uchambuzi na Mwandishi wa kitabu cha Wagalatia.**

**Rudi Nyumbani**

Share on:  
WhatsApp